



Ni wajibu wako ewe mwanamke wa Ki-islamu kumtii mume wako katika mambo mema. Abu Hurairah (Radhiallahu `anhu) amesema kuwa Rasoolullaah (Sallallahu `Alaihi Wasallam) amesema: **“Atakapo Swali mwanamke swala zake tano (daima) na kusitiri tupu yake na akamtii mume wake, basi ataingia Peponi kwa kupitia mlango wowote apendao katika milango ya Peponi.”** [Imepokewa na Ibn Hibbaan katika Saheeh]

Kutoka kwa Abu Hurairah (Radhiallahu `anhu), Rasoolullaah (Sallallahu Alaihi Wasallam) amesema: **“Hairuhusiwi kwa mwanamke kufunga (saumu) wakati mumewe yupamoja nae illa kwa ruhusa yake (mume). Na haifai (kwa mwanamke) kumruhusu mtu yeyote kingia katika nyumba ya mumewe illa kwa ruhusa yake (mume).”** [Bukhari na Muslim]

Vile vile kutoka kwa Abu Hurairah (Radhiallaahu `anhu) kuwa Rasoolullaah (Sallallahu `Alaihi Wasallam) amesema: **“Mume atakapomwita mkewe kitandani na asimuitike, naye apitishie usiku ilhali amemkasirikia mkewe, malaika humlaani (mke huyo) usiku kucha hadi kupambazuke.”** [Bukhari na Muslim]

Na katika riwaya ya Bukhari na Muslim, Rasoolullaah (Sallallahu Alaihi Wasallam) amesema: **“Naapa kwa Yule Aliyeiliki roho yangu, hakuna mwanamume anayemwita mkewe kitandani na amkatalie, isipokuwa yule Aliye juu ya mbingu humkasirikia mpaka mume wake amridhie.”**

Miongoni mwa hakki za mume juu ya mkewe ni (mke) kutekeleza mambo ya nyumbani na kutotoka nje ya nyumba bila ya ruhusa yake. Rasoolullaah (Sallalaahu `Alaihi Wasallam) amesema: **“Mke ndiye mlinzi wa nyumba ya mumewe na ataulizwa juu ya wadhifa wake.”** [Bukhari na Muslim]

Hakki nyengine ya mume juu ya mkewe ni kuwa (mke) atatekeleza kazi za kinyumbani na asimfanye mume wake kumuajiri mfanyi-kazi wa kike, jambo ambalo litakalo leta madhara ambayo yatakayo-muhatarishia uhusiano na watoto wake.

Shaykh ul-Islam Ibn Taymiyyah (Rahimahullaah) amesema katika kuyasherehe maneno ya Allaah yasemayo (kama yalivyofasiriwa):

فَأَصْلِحَتْ قَبِيَّتَكَ حَفِظْتَ لِلْغَيْبِ بِمَا حَفِظَ اللَّهُ

**Basi wanawake wema ni wale wenye kut'ii na wanao jilinda hata katika siri wakati waume zao hawako kwa kuwa Allah ameamrisha wajilinde (yaani tupu zao).** (Surah an-Nisaa 4:34)

“Hii inalazimu wajibu uliodhahiri wa mwanamke kumtii mume wake, katika mambo yote, kama vile kumtumikia, kusafiri nae, kumsaidia katika mambo mengine, kama ilivyotajwa kwenye Sunnah za Mtume .” **[Majmoo' al-Fataawa 32/260 – 261]**

Mwanachuoni mkubwa, Ibn al-Qayyim (Rahimahullaah) amesema: “Wale wasemao kuwa ni wajibu kwa mwanamke kumtumikia mume wake hutumia aya hii kama dalili kuwa wale waliopewa maamrisha na Allah (kuhusiana na tukio hili) wanachukulia jambo hilo kuwa ni katika al-ma'roof (wema). Amma kwa mwanamke anaestarehe na kumtumisha mumewe, na kufagia, kutwanga unga, kukanda unga, na kufua nguo, kutandika kitanda, na kutekeleza mambo ya kinyumbani, basi hayo yatakuwa ni katika al-munkar (uovu). Akasema Allaah Subhaanahu wata'aalah (kama ilivyofasiriwa):

وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ

**'Nao (wanawake) wanayo haki kwa Sharia (kufanyiwa na waume zao) kama ile haki iliyo juu yao kuwafanyia waume zao.'** [Soorah al-Baqarah 2:228]

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ

**“Wanaume ni walinzi na wasimamizi juu ya wanawake.”** [Surah an-Nisaa 4:34]

Basi iwapo mke hatomuhudumia mumewe, na badala yake (yeye mume) akawa ni kama kijakazi chake, hii itamaanisha yakwamba huyo mke ndiye mlinzi na msimamizi juu yake”

Akaendelea kusema: “Kwa hakika Allaah amemlazimu mume kumuhudumia mkewe ki-matumizi, kumnunulia mavazi na kumsimamia ili awe na mahala pa kuishi na kwa upande wake akawa anastarehe nae na kuhudumiwa, pamoja na yale ambayo yanayotekelezwa katika desturi za mume na mke.

Vilevile, mkataba wa harusi unahitaji kuwa mume na mke waishi kwa wema. Na maana ya wema ni mke kumtumikia (mumewe) na kutekeleza mambo ya kinyumbani.”

Na akasema: “Na hakuna tofauti yoyote inayombagua mwanamke iwapo ni mke wa fahari au duni, au awe ni masikini au tajiri. Hebu mtizame mwanamke huyu ambaye aliyemtukufu wa wanawake ulimwenguni ....” [al-Hadee 5/188-189]

Alikuwa amemkusudia Faatimah (Radhiallaahu `anha) kwani alikuwa akimtumikia mumewe na kuja kwa Mtume (Sallallahu `Alaihi Wasallam) kumlalamikia, walakin yeye hakuwa ni mwenye kulalamika juu yake (Faatimah).